

## **Fasihi Linganishi za Afrika**

Kamati ya Utafiti ya ICLA ya Fasihi Linganishi za Afrika ilibuniwa na William Spurlin na Marcio Seligmann mwaka 2019 ili kurekebisha ukosefu wa kamati ya fasihi za Afrika katika ICLA - fasihi za aina mbalimbali, na ambazo ni mionganoni mwa fasihi kongwe zaidi ulimwenguni.

Kinyume na watu wengi wanavyofikiria, fasihi za Afrika ni za kusisimua, zenyе ukwasi, na zina historia ndefu. Mipaka yoyote itakayofikiriwa — ikiwa ni ya kijiografia, kitanzu, kilugha, kihadhira au ya kimuhula — fasihi hizi zimeivuka na kuipita mipaka hiyo. Kutokana na kwamba bara la Afrika lina wakazi karibu bilioni moja, jumla ya nchi hamsini na nne, na aina mbalimbali za fasihi na utamaduni — katika bara lenyewe na pia katika diaspora ya Afrika kwa miaka elfu kadhaa, basi uwezekano na nafasi za kuwa na uchambuzi linganishi ni nyingi na zenyе changamoto. Kwa hivyo, lengo la hii Kamati ya Utafiti ni kutoa mchango wa kudumu katika fani ya tafiti linganishi, na wakati huo huo kusaili kwa kina mwelekeo wa kitaaluma unaoendelea kutumiwa, ambao huzitazama na kuzitathmini fasihi kwa jicho la Ulaya.

Kamati inawakaribisha wasomi wa fasihi za nchi yoyote ya Afrika (Kaskazini, Mashariki, Kusini na Magharibi) au diaspora ya Afrika — wanaohusika na fasihi za Afrika zilizoandikwa kwa lugha za kikoloni, pamoja na wasomi wa utanzu wowote wa fasihi maandishi na fasihi simulizi za lugha yoyote kati ya maelfu ya lugha za kienyeji za Afrika, na za karne yoyote. Lengo jengine la Kamati hii ni kuendeleza mijadala iliyoko kuhusu fasihi za Afrika na kuwawezesha wasomi kuwasilisha matokeo ya tafiti zao na kushirikiana nao katika kuyaboresha matokeo hayo. Hasa, Kamati ya Utafiti itakuwa inawasaidia katika usomi wao wasomi wa fasihi za Afrika wanaofanya kazi barani Afrika. Kutokana na kwamba katika bara la Afrika kuna makabila, tamaduni na lugha mbalimbali, Kamati hii ya Utafiti itahimiza usomi katika nchi na lugha nyingi iwezekanavyo. Baadhi ya mada zake ni kujikomboa kutokana na ukoloni, uhusiano wa fasihi na sanaa nyenginezo, jinsia na tafiti za LGBTQ, athari zinazoendelea za vita vya kutokomeza ukoloni na migogoro iliyozuka baada ya uhuru, Umajumui wa Afrika, diaspora ya Afrika, na siasa za tafsiri katika muktadha wa Afrika, na kadhalika.

Mtu yejote anayejishughulisha kitaaluma katika fasihi za Afrika, na hasa kwa kutumia mkabala wa ulinganishi katika usomi wa fasihi, historia, na tamaduni za Afrika, anaweza kuwa wanachama wa Kamati hii.